

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI CHIENJERE**

**SLP 120,**  
**RUANGWA,**  
**26/11/2020.**

**SCHOOL MOTTO: "EDUCATION WITH DISCIPLINE BRINGS SUCCESS"**

---

KUMB. NA . HWR/CHJSS/S.3908/F.1/21

NDUGU:.....

KIJJI CHA .....

SLP 51

RUANGWA.

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA I KATIKA SHULE YA SEKONDARI**  
**CHIENJERE MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kuijiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Chienjere mara baada ya kufaulu vizuri mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. **Hongera sana.**

Shule ya Sekondari Chienjere ipo katika Kata ya Chienjere Kijiji cha Chienjere umbali wa Kilomita 22.6 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

Shule hii ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wanafunzi wavulana na wasichana.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo (unapaswa kuzifanyia kazi na kuja nazo bila kukosa siku ya kuripoti Shule)

- ✓ Fomu namba 1 yenye orodha ya mahitaji muhimu ya Shule hii.
- ✓ Fomu namba 2 yenye Sheria na kanuni za Shule.
- ✓ Fomu namba 3 ya kupimwa na Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya/Kituo cha Afya
- ✓ Fomu namba 4 ya maelezo binafsi ya Mwanafunzi na Mzazi.

Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** na unatakiwa kuripoti Shuleni siku hiyo.

Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**

Mwisho nakutakia mafanikio mema hapa Shuleni katika kujielimisha na kumbuka kuwa, **ELIMU NA NIDHAMU HULETA MAFANIKIO**

Karibu Sana.

**SIMU:** Mkuu wa Shule 0787 065878, Makamu 0714 398194 , Mwl wa Taaluma 0682897037

**NB:** Sherehe maalumu ya kuwakaribisha kidato cha I itafanyika tarehe 23/01/2021. Mwandae mtoto wako mapema awahi kuripoti Shule.

**AHSANTE.**

.....  
**EUGEN M. LUDOVICK**  
**MKUU WA SHULE**

## MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

FOMU Na 1

### 1. SARE ZA SHULE

#### WAVULANA

- ✓ Suruali ndefu mbili (2) za rangi ya damu ya mzee zilizoshonwa kwa unadhifu na siyo na madoido. Suruali za kubana (modo) hazitakiwi. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi na kola shingoni. Tai mbili (2) ndefu za rangi ya damu ya mzee (Rangi inayofanana na ya Suruali). Mkanda mweusi kwa ajili ya kuvalia suruali, soksi nyeusi pea 2. Viatu vya ngozi vyeusi pea mbili vinavyofungwa na kamba. Fulana 1 (T-Shirt) yenye nembo ya Shule (Zinapatikana Shuleni).

#### WASICHANA

- ✓ Sketi mbili (2) ndefu (zinazovuka magoti) rangi ya damu ya mzee zilizoshonwa kwa unadhifu na kuwekwa marinda, hijabu nyeupe pea mbili (kwa atakayependa), (Nusu kanzu nyeupe kwa watakaovaa hijabu), Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi na kola shingoni (Kwa wasiovaa hijabu), Skafu mbili (2) ndefu (kwa wasiovaa hijabu) rangi ya damu ya mzee (Rangi inayofanana na ya Sketi), Soksi nyeupe pea 2 na Viatu vya ngozi vyeusi pea mbili vinavyofungwa na kamba (Viatu aina ya vibajaji haviruhusiwi). Fulana 1 (T-Shirt) yenye nembo ya Shule (Zinapatikana Shuleni).

NB: Tai na Skafu zinapatikana Shuleni kwa gharama ya Tsh 2,000/-

### 2. STAILI ZIFUATAZO ZA UVAAJI WA SARE YA SHULE HAZIRUHUSIWI

- ✓ Kushusha au kulegeza suruali (Mlegezo)
- ✓ Kuvaa sare ya Shule bila ya kuchekeka shati
- ✓ Kuvaa suruali bila ya kufunga mkanda
- ✓ Kuvaa sketi fupi ni kosa.
- ✓ Kuvaa viatu bila soksi ni kosa

#### MSISITIZO

Wazazi na wanafunzi wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kuhusu sare na uvaaji wa sare. Wakati mwingine wanafunzi kwa matakwa yao binafsi huamua kushona sketi fupi au suruali za kubana au zilizochongolewa. Ikumbukwe kuwa mavazi ya aina hiyo hayatakubaliwa. **EPUKA USUMBUFU NA KERO MAPEMA. ZINGATIA MAELEKEZO ULIOPEWA. UTAKAPORUDISHWA KWA SABABU YA YAKUTOZINGATIA MAAGIZO YALIYOTOLEWA USIJE KULALAMIKA AU KUMLAUMU MTU YEYOTE.**

### **3. VIFAA MBALIMBALI VINAUVYOHITAJIKA**

#### **(a) VIFAA VYA KUFANYIA USAFI**

Jembe 1 aina ya Ngwamba lenye mpini kwa wote, Ndoo 1 (Sado) kwa wote, (Wavulana panga lililonolewa na Wasichana fyekeo lililonolewa) na fagio aina ya Chelewa kwa wote.

#### **(b) VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

1. Daftari zisizopungua 12 (kaunta book) kalamu ya wino, penseli pamoja na mkebe wa hisabati ( mathematical set)
2. Karatasi nyeupe (ream paper) Bunda moja
3. Dictionary 1
4. Begi la kuhifadhia daftari
5. Mafaili mawili (moja kwa ajili ya kuhifadhi mitihani yako binafsi na la pili kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zake za kitaaluma hapa shuleni )

**NB:** Kwa mwanafunzi asiyekuwa na bima ya Afya (CHF au NHIF) anatakiwa kuchangia Shilingi Efu 5 (Tsh 5,000/-) ili apatiwe bima ya Afya.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

**Fomu Na 2**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo.

1. Kila mwanafunzi anapaswa kutumia akili na busara katika kufanya uamuzi wa vitendo mbalimbali shuleni. Kwa mfano kutohudhuria vipindi darasani ni kosa kuongea lugha za matusi ni kosa, kupiga kelele nje na ndani ya darasa ni kosa.
2. Kila mwanafunzi anapaswa kufika shuleni saa 12:50 asubuhi kwa ajili ya kufanya usafi wa mazingira na maandalizi ya kuingia darasani kwenye vipindi.
  - Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi kwenye eneo la paredi inapogongwa kengele
  - Kila mwanafunzi lazima awahi anapoitwa na kiongozi (mwalimu, kiranja au mfanyakazi mwingine)
3. Wanafunzi wanapaswa kuheshimiana wenyewe na kumheshimu mtu yeyote aliyewazidi umri kwa hiyo **NI LAZIMA KWA MWANAFUNZI KUSIMAMA NA KUSALIMIA WATU WAZIMA KWA KUTOA SHIKAMOO AU KUSALIMIA KWA KIINGEREZA ANAPOKUTANA NA MWALIMU WAKE.**
4. Ni kosa kwa mwanafunzi kuja shuleni bila kuwa na sare ya shule, labda kwa ruhusa maalumu. Ni marufuku kuvaa kofia, ndala, bangili, mkufu, hereni na pete **WASICHANA HAWARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.**
5. Siku za shule wanafunzi watatoka nje ya shule kwa kibali maalumu cha maandashi. Ruhusa itatolewa na mwalimu wa zamu. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule.
6. Kazi ni wajibu wa kila mwanafunzi kwa hiyo ni kosa kutofanya au kutegea kazi za mikono ambazo utakuwa umepangiwa na viongozi wako.
7. Ni kosa kwa wanafunzi kuonekana akizurura kwenye maeneo ya nyumba za kulala wageni (Guest house)
8. Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kufanya mgomo au kushiriki katika aina yoyote ya mgomo.
9. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu ya matusi, kashifa au kajeli.
10. Unatakiwa kukimbia unapoitwa au kutumwa na mwalimu au mtu mzima.
11. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wasiyo walimu bila ruhusa.
12. Ni kosa kwa mwanafunzi kugombana au kuchochea wengine wagombane.
13. Mwanafunzi ajjepushe na makosa yafuatayo ambayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja yakidhihirika.
  - Uasherati, Ubakaji/ushoga
  - Kuoja au kuolewa
  - Kupata mimba au kuharibu/kutoa mimba

- Kuwa na simu ya mkononi
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya au kuua
- Kumpiga mtu yeyote (kupigana)
- Utoro wa muda mrefu (Miezi mitatu mfululizo)
- Kukataa adhabu iliyotolewa na Mwalimu au Kiongozi
- Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- Wizi wa mitihani au kudanganya wakati wa mitihani ya aina yoyote
- Kujificha porini kwa lengo la kutoroka vipindi au Shule kwa ujumla
- Kudharau Bendera ya Taifa au Wimbo wa Taifa, Fedha na viongozi halali wa vyama na Serikali.

.....  
**EUGEN M. LUDOVICK**  
**MKUU WA SHULE**

FOMU Na 3

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Chienjere Secondary School,  
P.O.Box 120,  
**RUANGWA**

Date .....

Ref. No .....

**PART A:**

To The Medical Officer,

.....  
.....  
.....

REF: .....

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for being student for secondary school education.

1. (a) Eye sight  
(b) Hearing  
(c) Limbs  
(d) Speech  
(e) Venereal disease  
(f) Leprosy  
(g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Other serious diseases
4. Pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that he/she is physically fit or not fit for full time secondary school education.

- |                          |                                |
|--------------------------|--------------------------------|
| a) Eye sight .....       | f) Leprosy .....               |
| b) Hearing .....         | g) Epilepsy.....               |
| c) Limbs.....            | h)Neurosis.....                |
| d) Speech.....           | i)Other serious diseases ..... |
| e) Venereal disease..... | j) Pregnancy.....              |

Date ..... Signature .....Official Stamp.....

Station ..... Designation.....

## FOMU Na 4

### MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI

1. Jina la Kamili.....  
(Kama lilivyo kwenye orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga Sekondari)
2. Tarehe ya kuzaliwa. ....
3. Anwani ya nyumbani.....
4. Mahali unapoishi(nyumbani kwenu) : Wilaya. .... "Tarafa' ..... ' '  
Kata.. ..... '.....Kijiji.....
5. Shule ya Msingi uliyotoka.....
6. Dini.....
7. Kabila.....
8. Taifa(Mtanzania /Si Mtanzania)
9. Jamaa katika familia(Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)  
(i) Jina la Baba.....  
Anuani. ....Namba Ya simu.....  
Kazi yake.....  
(ii) Jina la Mama.....  
Anuani. ....Namba Ya simu.....  
Kazi yake.....  
(iii) Jina la Mlezi/Ndugu.....  
Anuani. ....Namba Ya simu.....  
Kazi yake.....
10. Mkataba wa Mwanafunzi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai  
Mimi. .. ..... (Mwanafunzi) nakiri kuwa, nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi ninaahidi: "Nitazifuata Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kama zilivyoelekezwa Aidha ninaamini kuwa Sheria na Taratibu zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu, maadili na taaluma." Vilevile naahidi kuwa sitoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidharnu zichukuliwe dhidi yangu.

Sahihi wa mwanafunzi .....Tarehe.....

11. Form ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na shule

Mimi.....(Mzazi/Mlezi)wa

Mwanafunzi..... **Ninakiri** kuwa, nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote yaliyotolewa na shule. Hivyo basi niko tayari mtoto wangu asome katika shule hii na nitakuwa tayari kumpa kila aina ya msaada utakaohitajika katika kufanikisha masomo yake na malezi yake kwa ujumla akiwa hapa shuleni kwa kipindi chote akiwa mwanafunzi.

Sahihi ya Mzazi.....Tarehe.....

***KARIBU SANA KATIKA SHULE HII***

**Sahihi ya Mkuu wa Shule.....**

**Jina la Mkuu wa Shule: EUGEN M. LUDOVICK**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule.....**